

## ***Karatu kupata maji ya uhakika ndani ya kipindi cha miezi miwili***

Serikali ya Awamu ya tano inayoongozwa na Mhe. Rais John Joseph Pombe Magufuli imetoa fedha kwa ajili ya kufufua mradi wa maji kwa lengo la kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa wakazi na kuchochea kukua kwa uchumi kupitia fursa iliyopo ya biashara ya utalii katika mji wa Karatu.

Hayo yamethibitishwa hivi karibuni baada ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha inayosimamia mradi huo kufanya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo unaogharimu shilingi 796,309,910 mil.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha Mhandisi Ruth S. Koya katika taarifa yake kwa Bodi amesema kuwa uendelezaji wa mradi huo utaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kutoka asilimia 33 ya sasa ambayo ni sawa na wakazi 7,500 wanaopata maji hadi kufikia asilimia 56 sawa na wakazi 10,404 wa mji huo watakaonufaika na mradi huo. “kazi hii imepangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi miwili ifikapo Mwezi Julai mwaka huu alibainisha Mkurugenzi wa AUWSA.



*Wakurugenzi wa Bodi ya AUWSA na Mwenyeji wao Mwenyekiti wa Bodi ya KARUWASA wakikagua kisima cha maji cha Bwawani Mjnini Karatu*

Katika taarifa yake kwa Bodi Mhandisi Koya alifafanua kuwa utekelezaji wa mradi huo umegawanyika katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa lita 225,000, ujezi wa tenki la kukusanya maji lenye ujazo wa lita 90,000 pamoja na jengo kwa ajili ya mitambo ya kusukumia maji

“Awamu ya kwanza pia itahusisha ununuzi wa Pampu mbili za kusukuma maji pamoja na kulipia gharama za kupeleka umeme kwa ajili ya kuendeshea mitambo ya uzalishaji maji katika mradi huo” alisema Mhandisi Koya.

Katika maelezo yake Mkurugenzi huyo wa AUWSA alisema kuwa kazi zilizotekelezwa mpaka sasa ni ujenzi wa tanki umekamilika kwa asilimia 90 na lipo katika hatua za mwisho kabisa za

kukamilika tayari kwa matumizi. “ujenzi wa teki kwa ajili ya kukusanyia maji kabla hayajaelekezwa kwenye tanki kubwa umekamilika na kazi zote za awamu ya kwanza zinatarajiwa kukamilika ifikapo Julai Mwaka huu” alisema Mkurugenzi huyo wa AUWSA.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa AUWSA awamu ya pili ya mradi itahusisha ulazaji wa bomba kwenda kwenye tenki eneo la “Linda Farm” na miundombinu iliyopo sasa kwa lengo la kuwafikishia wakazi wa Mji wa Karatu na maeneo ya pembezoni huduma ya Maji.



*Mwenyekiti wa Bodi ya AUWSA akizungumza na wananchi waliokuwa wakipata huduma ya maji katika kituo cha maji Mjini Karatu*

Awali Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi Mjini Karatu (KARUWASA) akimkaribisha Mwenyekiti wa Bodi ya AUWSA kukagua utekelezaji wa Mradi, alisema kuwa anashukuru sana kwa Serikali ya Awamu ya tano kusikia kilio cha wakazi wa Karatu na kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi wa maji iliokuwepo ambao ulizinduliwa na Mhe. Rais wa Awamu ya Nne kutokidhi mahitaji ya maji kwa mji huo.

Akitoa maelekezo ya Bodi Mwenyekiti wa Bodi ya AUWSA Daktari Mhandisi Richard Masika alisema kuwa AUWSA kupitia msimamizi wake katika mradi huo akishirikiana na Mhandisi wa Maji wa KARUWASA wahakikishe wanatekeleza wajibu wao kwa kumaliza mradi kwa wakati uliowekwa na kwa kiwango kilichopo kwenye mkataba na kwamba wanapima sampuli za vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa mradi huo.



*Tenki la Maji la ujazo wa lita 90,000 katika eneo la kwa Tom Mjini Karatu*

AUWSA inasimamia mradi wa Maji katika Mji wa Karatu kwa kushirikiana na KARUWASA baada ya kupokea maelekezo kutoka Wizara ya Maji ambapo mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2014 kwa kuwekwa jiwe la msingi na Mhe Waziri Mkuu wa awamu ya Nne Mhe. Mizengo Pindan a kuzinduliwa na Mhe Rais wa awamu hiyo Mhe. Daktari Jakaya Mrisho Kikwete mnamo mwezi Aprili, 2014.

----- MWISHO-----